

# Filemoni



# Contents

Shukrani Na Maombi1Maombi Ya Paulo Ya Kuntetea Onesimo1Salamu Za  
Mwisho Na Dua Ya Kuwatakia Heri2



# Filemoni

1Paulo, mfungwa wa Kristo Yesu,  
pamoja na Timotheo ndugu yetu:

sasa anakufaa sana wewe na mimi  
pia.

**K** wa Filemoni rafiki yetu mpendwa  
na mtendakazi mwenzetu, <sup>2</sup> kwa  
dada yetu mpendwa Afia, kwa Arkipo  
askari mwenzetu na kwa kanisa lile  
likutanalo nyumbani mwako:

3Neema iwe nanyi na amani  
itokayo kwa Mungu Baba yetu na  
Bwana Yesu Kristo.  
Shukrani Na Maombi

4Siku zote ninamshukuru Mungu  
ninapokukumbuka katika maombi  
yangu, <sup>5</sup> kwa sababu ninasikia juu  
ya imani yako katika Bwana Yesu na  
upendo wako kwa watakatifu wote.

<sup>6</sup> Naomba utiwe nguvu katika  
kuishuhudia imani yako, ili upate  
kuwa na ufahamu mkamilifu juu ya  
kila kitu chema tulicho nacho ndani  
ya Kristo. <sup>7</sup> Upendo wako  
umenifurahisha mno na kunitia  
moyo, kwa sababu wewe ndugu,  
umeiburudisha mioyo ya watakatifu.  
Maombi Ya Paulo Ya Kumtetea  
Onesimo

8Hata hivyo, ingawa katika Kristo  
ningeweza kuwa na ujasiri na  
kukuagiza yale yakupasayo kutenda,  
<sup>9</sup> lakini ninakuomba kwa upendo,  
mimi Paulo, mzee na pia sasa nikiwa  
mfungwa wa Kristo Yesu, <sup>10</sup>  
nakuomba kwa ajili ya mwanangu  
Onesimo, <sup>1</sup> aliyefanyika mwanangu  
nilipokuwa kwenye minyororo. <sup>11</sup>  
Mwanzoni alikuwa hakufai, lakini

12Namtuma kwako, yeye aliye  
moyo wangu hasa. <sup>13</sup> Ningependa  
nikae naye ili ashike nafasi yako ya  
kunisaidia wakati huu nikiwa  
kifungoni kwa ajili ya Injili. <sup>14</sup>  
Lakini sikutaka kufanya lolote bila  
idhini yako, ili wema wowote  
uufanyao usiwe wa lazima, bali wa  
hiari. <sup>15</sup> Huenda sababu ya yeye  
kutengwa nawe kwa kitambo kidogo  
ni ili uwe naye daima. <sup>16</sup> Si kama  
mtumwa, bali bora kuliko mtumwa,  
kama ndugu mpendwa. Yeye ni  
mpendwa sana kwangu na hata  
kwako zaidi, yeye kama mwanadamu  
na kama ndugu katika Bwana.

17Hivyo kama unanihesabu mimi  
kuwa mshirika wako, mkaribishe  
kama vile ungenikaribisha mimi  
mwenyewe. <sup>18</sup> Kama amekukosea  
lolote au kama unamdai chochote,  
nidai mimi. <sup>19</sup> Ni mimi Paulo,  
ninayeandika waraka huu kwa  
mkono wangu mwenyewe.  
Nitakulipa. Sitaji kwamba nakudai  
hata nafsi yako. <sup>20</sup> Ndugu yangu,  
natamani nipate faida kwako katika  
Bwana, uuburudishe moyo wangu  
katika Kristo. <sup>21</sup> Nikiwa na hakika  
ya utii wako, nakuandikia, nikijua  
kwamba utafanya hata zaidi ya yale  
ninayokuomba.

22Jambo moja zaidi: Niandalie  
chumba cha wageni, kwa kuwa  
nataraji kurudishwa kwenu kama  
jibu la maombi yenu.

<sup>1</sup> + 1:10 Onesimo maana yake ni Wa manufaa.

Salamu Za Mwisho Na Dua Ya  
Kuwatakia Heri

23Epafra, aliye mfungwa  
mwenzangu katika Kristo Yesu,  
anakusalimu. <sup>24</sup> Vivyo hivyo Marko,

Aristarko, Dema na Luka,  
watendakazi wenzangu  
wanakusalimu.

25Neema ya Bwana Yesu Kristo  
iwe pamoja na roho zenu. Amen.